# Lugha, Fasihi na Ukabila: Mwelekeo wa *Nasikia Sauti ya Mama*

*Deborah Nanyama Amukowa*
*Chuo Kikuu cha Maseno, Kenya*

**Ikisiri**

**Ukabila ni dhana ambayo inajidiliwa katika vyombo vya habari na wanasiasa na hata wananchi wa kawaida wameipa dhana hii nafasi katika mazungumzo yao ya kila siku. Hivyo basi, ukabila umekita mizizi katika harakati za maisha ya watu. Inaaminika kuwa dhana hii ilizuliwa na watu wachache wenye nia ya kukidhi matakwa yao kisiasa ili kujinufaisha na mfumo wa maisha ambao utawafanya watu wengine katika jamii kujiona wametengwa na kubaguliwa. Ukabila umesababishwa na ubinafsi wa watu wanaojiweka mstari wa mbele katika kutekeleza majukumu ya maendeleo katika jamii ambayo ina watu wenye mtazamo, itikadi, dini, lugha na tamaduni tofauti. Tofauti hizi husababisha jamii moja kujitenga na nyingine na kuibua matabaka ya watu ambao kila mmoja anajiona bora kuliko mwenzake. Makala haya basi yatajadili suala la ukabila kwa kurejelea riwaya, tawasifu/bayografia ya *Nasikia Sauti ya Mama* mintaarafu lugha ya Kiswahili iliyotumiwa katika utunzi wake.**

**Maneno Muhimu**: Fasihi, Lugha, Ukabila, Ujima.

## Utangulizi

Ukabila ni hali ya kimawazo inayomwongoza mja kuamini kuwa kabila lake ni la kipekee. Hali hii bila shaka humfanya mtu kuwa na kiburi. Akishakijaza kichwa chake kasumba hii, basi mapenzi yake kwa kabila lake hugeuka na kuwa chuki kwa yeyote asiyekuwa na 'bahati' ya kuzaliwa kwenye kabila hilo teule. Mwishowe huyu kiumbe atajenga imani kuwa kiongozi wa kabila lake asipotawala, wale 'wadhaifu' wa makabila mengine wataiharibu nchi. Huu ni upumbafu wa kiasi kikubwa sana (Oxford, 2018).

Hivyo basi ni dhahiri kwamba ukabila hausababishwi na maarifa ya mwanasiasa pekee. Ukabila ni hisia tunazozaliwa nazo. Mwanasiasa kwa ajili ya werevu wake hutafuta mafuta ya petroli akayanyunyiza kwenyemakovu ya ukabila na kuwasha kiberiti. Hapo ndipo moto wa chuki huwaka, naye mwanasiasa husalia akijigamba kuwa yeye ni fahali. Kwa sababu ukabila ni fikira

za kiasilia kutokana na maumbile ya kibinadamu, hata masomo hushindwa kuliondoa doa hilo. Aidha si jambo la kushangaza kamwe kuwaona vijana wachanga kwenye vyuo wakitapatapa kwenye huu uchafu wa kikabila. Wao hunena bila aibu kwenye mitandao kuwa kiongozi wa kabila lake ndiye anastahili kutawala nchi.

**Kuthamini Jamii: Kuishi kwa Ujima**

Mintarafu Walibora (2014), watu walithamini jamii zao na kuishi pamoja kwaujima.watotowalipewa majina iIi wapate utulivu baada ya kuzaliwa. Ni desturi iIiyokuwa na umuhimu mkubwa katika maisha ya wanajamii. Mtoto alipendekezewa majina kadha huku akilia. Hii ilikuwa orodha ndefu ya wahengawa jamii husika waliokwishafariki. Jina lililotajwa na papo hapo mtoto mchanga akanyamaza huwa ishara ya mtoto kukubali jina la mhenga aliyetajwa. Hali hii inadhihirisha kuwa wanajamii wote walithaminiwa biIa kujaIi kama kuna uhusiano wa karibu sana kifamilia au la.

> Kwake Bibi, jina Atanasi lilikuwa na umuhimu mkubwa kwa Atanasi alikuwa hayati babu yake ambaye kazaliwa ,kuishi, na kufia Uganda Mashariki. Nalo jina Waliaula lilikuwa mmojawapo wa watoto tisa wa wa kiume wa mwanzilishi wa ukoo wetu wa Bakokho mwenye jina Wambete. uk.17

HaIi hii hufanya wanajamii kujivunia jamii nyinginezo na kuondoa hisia za ubaguzi. Hivyo basi, msimulizi alipoambiwa kuwa alikuwa na jina lingine akiwa na umri wa takriban miaka mitano, alifurahi mno ilhali halikuwa na uhusiano wowote na jamii yake.

> NiIivutiwa sana na jina Kennedy kwa vile niligundua lilikuwa jina la familia moja maarufu nchini Marekani ambamo wote waliondokea kuwa marais na viongozi wa kutajika. uk .17

Watu waIiishi kwa ujamaa na kujivunia ufanisi wa kila mmoja wao. Kupitia masimulizi ya msanii, jamii yake ni kubwa lakini uhusiano katika kila kiwango ni muhimu. Baada ya jamii ya Bakokho kugawika mara mbili, kikundi kimoja kilielekea Matili karibu na mji wa Kimilili. Katika kundi hili alikuwemo Mzee Masinde aliyekuwa babuye mwanasiasa maarufu Masinde Muliro katika historia ya Magharibi mwa Kenya. Alifiwa wazazi wake akiwa bado mtoto mdogo na akalelewa na nduguye wa kambo. Babuye Msimulizi alichangia masomo ya Muliro. Urafiki pia uIichangia kuishi kwa amani. Ubaguzi haukushuhudiwa iIhaIi kuna watu wengine katika jamii waIiopata ufanisi mkubwa maishani baada ya kupata eIimu mfano wa Babake Msimulizi na Masinde Muliro. Badala ya chuki wanajamii walitamani kushirikiana nao hata kwa kuwapa salamu tu. Mawazo haya ni ithibati kuwa fasihi ni sehemu ya jamii na kupitia kwayo jamii hupata suluhu ya matatizo yanayoikumba, Mulokozi (1996).

> Babu Muliro hakuwa mtu wa nasaba tu bali pia rafiki wa Baba wa kufa kuzikana hasa. uk 20.

Wakati wa uchwejua waIishirikiana na kuhakikisha kuwa kiIa mwanajamii anaikimu famiIia yake. WaIiombana hata vijinga vya moto kutegemea nani meko yake yamewaka na ya nani yamezima. Waliishi kama jamii moja huko wakipewa mahali pa kulima na kuzalisha vyakula. Hata hivyo wanawake waItamani kupata mashamba yao wenyewe ili wajitegemee.

> Mama katoka kwa Mama Joan na kijinga cha moto. Anasindikizwa na binamu yake Joan huku wakisemezana na kuelezana matamanio yao. Lini mwenzangu nasi tutawahi kupata mashamba yetu wenyewe sisi na waume zetu?...Natamani ije leo au kesho… Mungu atujalie tupate mashamba yetu wenyewe tupandikize migomba ya ndizi watoto wetu wale washibe.uk.23.

Je, ndio mwanzo wa ukabiIa? Ni dhahiri kuwa katika ujima kuna changamoto. Baadhi ya wanajamii hutaka kumiliki mali yao kama watu binafsi. Hata hivyo, katika makazi ya watu kutoka katika jamii tofauti, palijaa ushirikiano na amani. Kulingana na nadharia mpya ya uhakiki wa fasihi, kila jamii huendeleza fasihi ambayo huifaidi na kuiwezesha kuishi kwa umoja na upendo, Musheyenzi (2003). Hivyo basi mchanganyiko wa watu katika makazi haukuzua mtafaruku wowote kama inavyodhihirika:

> Nilikimbia kutoka kwetu nikapita nyumba aliyoishi mwanariadha wa Olimpiki Cosmas Siele niliyekuwa nikila ugali kwake mara nyingi, nikapita makazi ya mwalimu Njoroge, naibu wa mwalimu mkuu, nikapita makazi ya mwalimu mkuu wa Chuo cha Walimu, Bwana Owino, nikapita kwa Kanani mwalimu mmoja wa Chuo cha Walimu…uk 64.

Vijana waliowinda wanyama kama vile sungura, swara, mbogo, mburukenge, kongoni,,tandala na nungunungu waliandamana na mbwa wa majirani bila ruhusa ya wamiliki wao.Hii ni njia majawapo ya kuonisha maendeleo ya kiutamaduni na kijamii kupitia mtazamo changamano kupitia fasihi.Pia ni hali ya jamii kujielewa na kujiamini kupitia itikadi za kijamii na kitamaduni zinazofungamana na hali mbalimbali za jamii husika kwa mujibu wa Senkoro (2011).

> Gitau wa Gathumbi alikuwa na mbwa wawili, Chux na Box waliokuwa mahiri sana katika uwindaji. Ulipaswa tu kuwaonyesha mahali swara alipopitia awali na mara moja wananusa harufu yake na kuandama nyayo zake mpaka wanamtimua na hatimaye kumkamata. Ila mbwa aliyekuwa hodari zaidi alikuwa Simba wa mama mmoja aitwaye Timna,… Tukimwita mbwa wake Simba kwa kupiga mbinja naye akishafika twaondoka naye…uk.118-119

Hata hivyo, katika jamii hizi kulikuwepo na watu wenye wivu waliohatarisha maisha ya wengine na kuzua mtafaruku. Huweza kusababisha vifo ambavyo

hutokea hasa kwa wale ambao huonyesha matumaini makubwa ya kufaulu maishani. Kisa cha kifo cha nduguye Msimulizi kinatilia shaka ujima. Yamkinika kuwa ndoa za wake wengi au ndugu wa kambo huhujumu ujima.

> Yanasemekana Wamukota alipewa sumu na mke wa ndugu wa kambo wa baba ambaye ilikuwa ni ada kwake kuyakatisha matumaini ya watu wengine walioonekana kufanikiwa… baada ya kakangu kufa na kuzikwa na matanga bado hayajamalizika, mtekelezaji njama alipania pia njama ya kunimaliza .uk 26-27.

Hili huwafanya baadhi ya wanajamii kujitenga na wengine. Hulazimika kuhama na hata kuishi mijini ili kuzisalimisha familia zao. Hali hii ilimsukuma babake msimulizi akahisi kuwa kijiji cha Baraki hakiwezi kuiweka familia yake tena. Hata mamake ambaye tangu kitambo akitamani kuwa na shamba lake mwenyewe alihuzunika mno na akatamani kuhama. Kiujumla, fasihi huambatanishwa na maendeleo, utamaduni, utambuzi nafsi na kwa ujumla kuipevusha.Mafanikio ya mikondo mbalimbali ya maisha inayochukuliwa na jamii yoyote hutegemea uelewekaji wa jamii katika wingi wake, Mutembei (2012).

> Kitumbua chake kilikuwa kimetiwa mchanga. Hakutaka tena aila yake kuendelea kustakimu kwenye ardhi ile ya Baraki iliyokuwa na watu wema na vilivile mahasidi waliokuwa tayari kufanya lolote kutuhiliki. Baba akawa hana budi kusalimu amri na kufunga virago na kutugurisha hadi mtaa wa Shauri Moyo, mjini Kitale kutoka Baraki alikozaliwa yeye pamoja na sisi watoto wake watano… kasoro mmoja aliyepigwa pute kwa vipengele vya husuda na sihiri. uk.27-28.

Jamii hii haikuruhusu wana wao kuzuru eneo la Baraki kwa muda mrefu. hata waliporuhusiwa ilikuwa ni kwa tahadhari nyingi mno.

> Usikubali kunywa wala kula chochotekwa mwafulani. Usikubali. Hatutaki mjifie mapema tukuzikeni nyie wazazi wenu, nyie ndio mpasao kutulilia na kutuzika tuzeekapo na kujifia. uk 30

Kuishi kwa ujima huwafanya watu kutambua kuwa mtu hawezi kuishi peke yake duniani na kila wakati kila mmoja anapaswa kumfikiria mwingine. Fasihi inakubalika kama chombo cha maendeleo katika jamii. Kuchunguza fasihi kwa mujibu hali halisi katika jamii kua faida mno. Juhudi hizi zinaweza kuipa fasihi msukumo mpya na kuifanya itumike kama njia mojawapo kupunguza ukabili katika jamii, Wamitila (2000,2008).Mamake msimulizi alisisitiza kila mara:

> Je, dunia inakuzungukia wewe mtu mmoja? Jua likuwakie wewe tu au mvua ikunyeshee tu wewe mtu mmoja? Tangu lini? uk.47

Ni kweli kwamba dunia ina watu wanaozungumza lugha mbalimbali. Hakuna mtu anayetarajia kuwa kila mtu atazungumza lugha yake. Mathalani Cherangani

nyumbani kwa msimulizi kuliishi watu wa makabila mengi kama vile Wakalenjin, Wakisii, Wateso, Wabukusu, Wakikuyu, Waturukana na wengine wengi. Utamaduni wa jamii hizo ulitofautiana. Isitoshe, kila jamii ilikuwa na kaida, mielekeo, misukumo, upungufu na ufanisi wao isipokuwa watu wote walipumua hewa waliyojaliwa na Mungu.

> Kulikuwa na hisia fulani na furaha katika mseto wa jumuiya ya watu watu wa Cherangani. Je ni kwa sababu watu wa Cherangani kutia ndani kabila la Wacherangani walijiona kwanza kuwa wanadamu na Wakenya kabla ya kjiona kuwa sehemu ya kabila lao au mbari yao? Je walijihisi kuwa watu wa kabila moja la Wakenya au wanadamu? Sijui, ila nilivyoona mimi palikuwa na mwanana na itifaki njema baina ya makabila yote. uk 48.

Mila na desturi za baadhi ya wanajamii ziliwashangaza baadhi ya Wanacherangani lakini hali hiyo haikuwakera. Mmoja wa wakazi anayetajwa kama mke wa Otieno aliajabia mila za jamii ya Wabukusu kuwaimbisha watoto mkesha wa siku ya tohara na kuwatembeza wakiwa uchi huku wamepakwa tope la mtoni na kutahiriwa kadamnasi. Msimulizi naye alishtuliwa na sauti za mingurumo ya simba nyakati za usiku baada ya wavulana wa Kinandi kutahiriwa mwituni ili wasionekane na wanawake na watu wasiokuwa wa kabila lao. Hata hivyo hali hii pia ilimvutia kutokana na ujasiri waWanandi katika kufuata desturi zao. Waliishi mwituni hadi walipopona na baadaye kufanyiwa matambiko ya miviga na desturi nyingine zilizoambatana na desturi za Kinandi. Fauka ya hayo kuna changamoto zilizoambatana na desturi za kutahiri wavulana miongoni mwa Wabukusu. Kuna wale ambao wangefanya usihiri na kusababisha madhara kama vile ngariba kukata uume wote, kushindwa kukata govi au govi kumea tena mara tu baada ya kukatwa. Hili wazo linashadidiwa na ujumbe wa Nambuye. Hali hii pia huhujumu ujima na kutenga watu wa jamii moja.

> Alikuja na ujumbe kutoka kwa bibi wa kuukeni… Kasema bibi kapata ufifi kwamba watu wenye nia mbaya walikuwa wamekula yamini kwamba nitayarishwapo kwa babu nitafia papo hapo kwa kutokwa na damu bila kukoma au kwa ngariba kunitahiri visivyo…Mama aliposikia habari zile akashadidia msimamo wake kwamba Baraki sirudi tena uk.124

Hata hivyo kuishi kwa ujima na kujali maslahi ya kila mtu huwa na madhara wakati mwingine hasa mtu anapojaribu kutenda wema katika jamii au miongoni mwa watu ambao hawamfahamu Senkoro, (2011). Hivyo basi katika jamii mtu anapokuwa na hulka njema, kanuni thabiti na msimamo usiotetereka sharti afanye hivyo miongoni mwa watu wanaomfahamu la sivyo huweza kumletea masaibu na mashaka na hata kuhatarisha maisha yake aliposhambuliwa na kutuhumiwa

kwa wizi wa ng'ombe. Hali hii ya kuthamini ujima ilimzalia Babu Makali balaa kama alivyosimulia mama.

> Siku moja babu yako Makali alikwenda mbali asikojulikana kutekeleza shughuli za kanisa…Akabaini kuwa huenda ng'ombe wameingilia mahindi ya mtu wanayala…aliamua kuingia shambani kwa mtu asiyemjua kuondoa hao ng'ombe… Ghafla akatokea mwanamke mmoja na kupiga kamsa. Uwiiii mwizi wa ng'ombe. uk.36-37.

Malezi ya watoto yalikuwa jukumu la kila mwanajamii. Mtoto alipokosa mtu mzima aliyekuwa karibu alichukua jukumu la kumwadhibu. Hili linatokea mtunzi anapopenyeza kijiti kwenye nyanya za baiskeli ya aliyetemka kwa baiskeli kutoka kwenye mwinamo wa mlima. Uchu wa uvumbuzi ulikuwa umemwingia na hakutaka lolote limpite. Mtu yule aliyumbayumba na kushuka kisha akavunja kijiti na kumcharaza viboko. Alipomfikisha nyumbani alipokelewa na mama kwa kichapo tena. Hii ni njia ya kuwafunza kuthamini kila mtu katika jamii. Hivyo basi watoto hukua bila kuwa na hisia za ubaguzi ambazo hatimaye huzaa ukabila.Watoto pia hujifunza kuishi na wenzao kwa amani kama Msimulizi na binamu yake Truphena.

> Kuja kwa Truphena , mkoi wangu kuliongeza mawanda ya ulimwengu wangu… Nilicheza naye mwajificho, foliti, kodwe, msakemke wangu, ..mchezo wa baba na mama. Tukachuma matunda mwitu na yasiyo mwitu kwa jirani yetu James Nalianya. uk.45

Wanajamii pia hutambua kuwa kutilia maanani haki za watoto ni jukumu la kila mwanajamii Senkoro (2011). Mtoto ni wa mama akiwa tumboni lakini punde tu anawapozaliwa ni wa jamii nzima. Ithibati ni namna umati wa watu ulivyomvamia mama mzazi aliyemwadhibu mwanawe vibaya kwa kukosa kurudisha masalio ya pesa baada ya kutumwa dukani. Alimshurutisha avue nguo zote, akamfunga kwa kamba na kuanza kumripua kwa mjeledi wa ngozi. Alitokwa na damu kila mahali kisha akaanza kuchuma pilipili na akajaribu kumweka machoni kama njia ya kumwadhibu. Alilia kwa uchungu.

> Kufumba na kufumbua umati wa watu ulikuwa umefunika mji wa mama yule. Haikutegemea kabila. Wanakijiji walitambua kuwa mama katendesa katika kumwadhibumwanawe…Meja alimpokonya yule mama mjeledi …Watu wengine wakamfungua kijana …Kisha ghafla bin vuu tukamwona Meja anamwangushia mjeledi mkali mgongoni. Yule mama akapiga ukemi na mkubwa..Meja aliendelea kuwaangushia mijeledi hadi hadi wanakijij walipoingilia kati na kumwambia ''Tosha''. uk 52.

Hivyo basi, mtu mmoja anapofanya kitendo kisichostahili huathiri jamii nzima. Kupitia hadithi ya mama Zambukuku katika jamii ya Babuya aliyemwadhibu mwanawe kwa kuwa nambari moja mwishoni mwa muhula.

Hakutarajia maelezo zaidi ila kumpiga yule kijana hasa kichwani huku akifoka kuwa kijana alikuwa nambari moja tu!!. Kijana alizirai na hatimaye kukata roho. Mauaji haya yameharibu sifa za jamii hii ya Babuya kuwa ni jamii mbaya kwa vile wao huadhibu watoto kwa kupiga kichwa. Kuna wimbo maarufu mwiongoni mwa jamii ya wabukusu ambao huimbwa wakati wa tohara: *Babuya Ekholo embi-Babuya ni ukoo mbaya*, tukio la mwanajamii mmoja limeipa jamii hii sifa hasi.

Jamii zinaposhirikiana na kuthaminiana huishi na kujali maslahi ya wengine kama watoto wa mtu mmoja. Watu wanaodhihirisha mapenzi wakati wa msiba. Mfano ni kifo cha Mzee Boi na mjukuu wa Jackson jirani wa msanii kule Cherangani vilihuzunisha kila mtu; si wanawake, si wanaume, si watoto, si watu wazima. Pia mshindo wa vilio uliotokana na tangazo la redio la mauaji ya mwanasiasa maarufu nchini Kenya la Julai 5, 1969. Mauaji ya kisiasa yaliyofuata yalibainisha mkondo wa kikabila baada ya vifo vya Ronald Ngali, mwaka wa 1972 na J. M Kariuki mwaka wa 1975. Je huo ndio uliokuwa mwanzo wa ukabila nchini Kenya?

**Aina Mpya ya Ukabila**

Hali ya maisha imezua kundi jipya na mwelekeo mpya kuhusu ukabila. Kutokana na ukosefu wa ardhi kulikuwa na wavamizi wa msitu wa serikali kwenye mwinamo wa vilima vya Cherangani na kuufanya makao na kupaita Shauri Yako. Chifu alitilia maanani operesheni ya serikali kuwahamisha wavamizi hao ambao walikuwa maskini wasio kuwa na makazi. Katika shughuli hiyo mkazi mmoja aliyeitwa Sabuni alikufa na kuzua maana mpya ya ukabila.

> Hakufa kwa sababu ya kabila lake la Kibaluhya au jina lake la Kiswahili bali kwa sababu ya kabila lake la walalahoi huku wenzake wote wakifurushwa kabisa kutoka eneo hilo. uk.51.

Hali hii inadhihirika pia kutokana na makazi ya wafanyakazi wa shule ya St. Joseph’s. Msimulizi anaeleza kuwa kulikuwepo na kambi ya wafanyakazi hohehahe kama vile walinzi, wapishi na wafagizi. Hali hii ya tofauti haikiwa ya kikabila bali ya kitabaka. Mbali na kukosa kuelewana kwa wakati fulani, hapakuwa na tofauti kubwa kati ya watu wa kambini na wale walioishi katika makazi ya walimu. Mtunzi anakiri kuwa babake hakuweza kununua baiskeli hadi palipotokea dharura ya nduguye msimulizi kuingia shule ya sekondari mbali na nyumbani. Aina hii mpya ya ukabila pia ilidhirika kupitia aina fulani ya maradhi. Mwandishi anasimulia kisa cha Mbugua kuzirai na kugunduliwa aliugua kifafa. Wanafunzi wenzake waliamini ni ugonjwa wa kuambukiza na kumwambaa kabisa. Tukio hili ni dhihirisho kuwa fasihi huweza kufunza jamii na kubadilisha mambo yalivyo katika jamii. Isitoshe, ni dhihirisho kuwa jamii yenye ujima hukumbwa na changamoto ambazo sharti zishughulikiwe kwa njia maalum,Wamitila(2000).

> Hakuna aliyetaka kumkaribia Mbugua. Walimwachia dawati akakaa pekee yake. kama kisiwa katikati ya bahari. Hakuna aliyetaka kumsalimia mkononi wala kusema naye. Akigusa chotechote, si kitabu, si kalamu, si mkoba, aliachiwa kama kwamba kakitia najisi isiyotakasika. uk.79

Baadaye Msimulizi alifunzwa na babake kuwa huo haukuwa ugonjwa wa kuambukiza ndipo akamfanya Mbugua rafiki wa karibu. Hata familia ya msimulizi ilimkaribisha kila mtu katika makazi yao bila kujali nasaba yao. Siku moja babake akamwokota Henry Muchelesi aliyekondeana na kuonekana kama aliyetoka kaburini. Baada ya kumkarimu kwa chakula alipelekwa shambani kumsaidia mamake kazi kwa muda wa zaidi ya mwaka mmoja alipoondoka na kwenda zake bila taarifa. Hakuna aliyelalama.

> Henry Machelesi kakaa kwetu shambakwazaidi ya mwaka mmoja Kisha asbuhi moja alivaa kaptura yake ya nili … Alijitwika sanduku lake la mbao na kwenda zake uk.68.

Ujima ulirahisisha kazi shambani. Watu walishirikiana kiasi cha kufanya kazi nyingi kwa muda mfupi bila kujali asili ya wenzao. Walifurahia kazi huku wakitumia vizimuo vya masimulizi au kuhadithiana.

> Tulikuwa watu wengi sana, majirani, wafanyakazi wengine walioajiriwa na mama, wakubwa zangu, watoto wa shangazi yetu Selina, aila ya Phares Simyiu, … Siku hizo watu wakifanya kazi ubia ilikuirahisisha katika roho ya utangamano wa kijamii iliyotamalaki. uk.67-68.

**Kupata Makazi**

Hapakuwa na ubaguzi wa kuptata makazi. Watu kutoka jamii mbalimbali wangehamia popote na kujipatia ardhi bila vita wala kununua. Mtu alifika mahali na kusema:

> Hapa pangu kutokea kwenye mwembe huu hadi mbuyu ule, na wewe ndugu yangu waweza kuchukua sehemu iliyosalia hadi kwenye ukingo wa mto.uk.21.

Hata wakati wa kugawa mashamba yaliyokuwa ya masetla hapakuwa na ubaguzi. Mchakato huo haukuwa na mapendeleo kamwe. Aliyehitaji shamba alichukua karatasi katika debe la bahati nasibu kupitia Mpango wa Makazi wa Suwerwa. Hatimaye familia ya Msimulizi ilihamia shambani na aliyetoa gari la kuwahamisha alikuwa Mathenge mwenye asili ya jamii ya wakikuyu.

**Elimu kwa Wote**

Wanajamii walitoa ardhi kwa minajili ya ujenzi wa shule kwa manufaa ya watoto wote katika jamii. Babuye Msimulizi alikuwa msitari wa mbele miongoni mwa wanaharakati wa awali kutetea haki ya watoto wa Kiafrika kwenda shuleni na kupata elimu wakati wa enzi ya wakoloni. Shule ya upili ya Bokoli inasimama

kwenye ardhi ya iliyotolewa naye kwa ushirikiano na watu wengine katika jamii yake.

Babake msanii hakubagua kwa upande wa kumtia adabu alipokosa akiwa shuleni. Hali hii iliwafanya wanafunzi wengine wasihisi kuwa walibaguliwa. Kisa cha Msimulizi na Muigai kinaeleza vyema walipofumaniwa wakitaka kupigana. Aliwashika na kuwapeleka ofisini na kuwaamuru wapige magoti kisha akawafungia pale kwa muda. Aliporejea kuwafungulia mlango, walikuwa wamepatana. Waliadhibiwa kwa viboko vitano kila mmoja wao. Walisalia marafiki hadi walipokamilisha masomo yao ya shule ya msingi.

***Nasikia Sauti ya Mama***

Mama ndiye aliyekuwa mwalimu wa kwanza kufunza mtoto kuhusu usuli wa jamii yake. Msanii wa *Nasikia Sauti ya Mama* alifunzwa kuhusu jamii yake. Ajifunza mengi kutokana na masimulizi ya mama. Msimulizi ameeleza kwa uketo wa lugha inayosisimua. Watu waliishi pamoja na kushiriki katika ndoa bila kujali usuli. Watu wangeweza kushiriki ndoa za mchanganyiko/mseto. Hata pale ambapo walishiriki katika vita kati ya jamii hizo, wasichana walitekwa nyara na kuozwa hivyo basi kuleta amani. Hata wasichana hao walibadilishwa majina na kupewa majina ya jamii ya waume wao. Hali hii inashadidiwa na maelezo ya mtunzi kuhusu familia ya Mzee Nambafu na watoto wake Patrick, Luka, na Mutenyo waliokuwa na mama wa kambo kutoka Uganda aliyekuwa na vitimbi visivyoelezeka. Pengine vilihusiana na desturi za jamii yao.

> Nakumbuka usiku mmoja alipoteta na Mzee Nambafu kisha kutahamaki kavua nguo zake zote na kutoka kambini walikoishi na kuja kuketi nje ya nyumba yetu.uk.81

Alice Hopf alikuwa Suriama aliyetokana na baba Mjerumani na mama Mwafrika mweusi kutoka viungani mwa mji wa Kitale. Naye babuye Msimulizi alikuwa na usuli wenye utata ambapo mamake alikuwa msichana wa Kijaluo aliyepewa jina la kibukusu. Pia urithi wa wanawake ulikuwa jambo la kawaida mume alipofariki na kuacha mke mwenye umri mdogo.

Uhasama wa kushambulia na kuua watu haujaanza hivi kambuni. Hali hii ilibainika hata mwanzoni mwa miaka ya 1900 mjombake alipouawawa akiwa safarini kwenda Uganda kutafuta ajira kwenye jeshi bila kisa na maana. Hii ilikuwa ishara ya ubaguzi.

Kupitia masimulizi ya Mama pia ni dhahiri kuwa dini ya Kikristu iliweza kuleta mabadiliko katika jamii kwa kuelimisha wanajamii k.v. Babu Makali ambao kwa ukarimu wake aliwaendeleza nduguze kimasomo na kuinua jamii yake bila mapendeleo na wakaweza kujitegemea maishani. Hali hii ilifanya familia hii kuishi kwa amani. Mafunzo ya mama kwa watoto wake husheheni mambo mengi. Muhimu ni kuwafunza watoto kuishi na kila mtu kwa amani bila ubaguzi na kuwa heshimu kwa kila hali.

> Mama alinizoea mimi nawakubwa wangu kuheshimu tamaduni mbalimbali na kutokuwa kabisa na kiburi cha kikabila wala dharau kwa wengine. Alisisitiza kuwa ingawa watu walikuwa na vimo tofauti , na rangi tofauti, na lugha tofauti sote binadamu tulikuwa na usuli mmoja yaani shamba la Edeni. uk.53

Mama daima ni mwombezi wa familia. Ukabila ulipokodolea nchi ya Kenya macho, mamake mwandishi aliomba bila kukoma. Amani ni muhimu katika kwa malezi ya watoto na maendeleo ya jamii kwa ujumla. Jamii nyingi za Kiafrika zinashililia kuwa mwanamke ana nafasi muhimu kaika maendeleo. Hivyo basi, fasihi imempa nafasi maalum.

> Je, Kenya itajiangamiza yenyewe kwa ukabila kama mtu anavyojiua kwa mikono yake mwenyewe kwa kujitia kitanzi?. uk.56

Usemi huu ni dhihirisho kuwa ukabila husambaratisha mambo mengi katika jamii. Wasiokuwa na hatia huathirika. Wananchi huishi katika hofu kuhuhsu mustakabali wa nchi katika siku za usoni. Mtunzi wa fasihi ana fursa ya kuangazia masuala haya na kupendekeza suluhisho. Walibora (2014) amebainisha hali hii kupitia usanii wa *Nasikia Sauti ya Mama.*

**Nafasi ya Kiswahili katika Vita Dhidi ya Ukabila**

Katika makazi mapya ya mseto wa jamii, Kiswahili kilitumiwa kama lugha ya mawasiliano hivi kwamba mahali palipovamiwa na wakazi katika msitu wa serkali paliitwa Shauri Yako, jina la Kiswahili lenye maana ya juhudi za mtu binafsi kujitetea iwapo patatokea jambo. Pia jina la mtu kama vile Sabuni ni ishara ya athari za lugha ya Kiswahili. Shuleni, hotuba za mwalimu mkuu na naibu wake zilikuwa katika lugha ya Kiswahili. Msimulizi alishangaa kwa sababu Kiswahili hakikuwa mojawapo ya masomo yaliyotahiniwa katika mtihani wa kitaifa. Walimu hawa walikuwa wanabainisha fahari na thamani ya lugha ya Kiswahili. Mwishowe ilibainika kuwa Kiswahili kilidhirisha sura ya uafrika. Utambulisho huu kupitia Kiswahili uliondoa fikira za kikabila jambo ambalo halikuzingatiwa na wizara ya elimu wakati huo.

> Hata hivyo hapana shaka kwamba wakati wizara ilipozuumu kujenga na kuwaumba vijana kama wazungu kasoro ngozi, Waafrika wanaochukia kuwa Waafrika, wanaochukia lugha zao, wanaochukia majina yao na asili yao…uk 75.

Kwanza, Kiswahili kilitekeleza wajibu huo kwa kuziunganisha dini za Kikristo na Kiislamu, hali ambayo imebuni mshikamano wa pamoja na uhisi wa kitaifa miongoni mwa wakazi wa kanda ya Afrika Mashariki. Hili linadhihirika kuwa kwanza, Kiswahili kilihusishwa na matumizi ya utoaji mihadhara katika misikitini, kabla ya kukubalika na Wakristo, na kuanza kutumika katika mahubiri katika makanisa. Itafahamika kuwa, eneo la Pwani ya Afrika Mashariki

liliukumbatia Uislamu kwanza, hata kabla ya kuja kwa Wamishenari, hali ambayo inatajwa kuanzisha mchakato wa kuondolewa mbali ukabila.

Kiswahili kimekuwa kikitekeleza jukumu muhimu katika uondoaji wa dhana hasi za kikabila tangu kuchipuka kwake na kukubalika kama muunganishi wa raia wa kanda ya Afrika Mashariki. Hata hivyo, ni muhimu kufahamu kuwa hata makabila makubwa na ya jadi yalikuwa na msingi wake uliozipa asili yake halisi ya "ukabila" ambao kimsingi ndiyo ulioipa utambuzi jamii hiyo. Kulingana Mazrui na Mazrui (1998), utaratibu wa uondoaji wa dhana za kikabila si hali ambayo kundi la watu husahau kujitambua kama Waluo, Wabaganda, Wakongomani au Wachagga kama wengi wanavyochukulia. Kulingana nao, kuna ushahidi mdogo sana kuwa licha ya dhana hasi za ukabila kuwepo, jamii za jadi zimesahau kujifikiria kwa misingi ya tamaduni zinazohusiana na lugha zao. Kwa mantiki hiyo, uondoaji wa dhana hasi za kikabila unapaswa kuchukuliwa katika muktadha tofauti.Hali hii inaweza kuchukua mkondo wa mabadiliko ya kimitindo, tamaduni na kanuni zinazoitambulisha jamii husika. Ufasiri halisi wa utaratibu huo ni kuwa hali hiyo hutokea wakati tamaduni za jamii zinabadilika na kuingiliana au kutagusana na a tamaduni nyingi (Senkoro, 2011) .

## Hitimisho

Ukombozi wa kwanza, tuliwafukuza walowezi kutoka Uropa tukajivunia kuwa waafrika huru. Ukombozi wa pili, tuliamua kujitawala kwa njia ya vyama vingi vya kisiasa. Tukasherehekea demokrasia. Ukombozi wa tatu utapatikana pale ambapo Wakenya watashinda vita dhidi ya ukabila na kuwachagua viongozi kwa vigezo vipya. Hapo ndipo taifa la Kenya litastawi kwa kiasi cha kila mwananchi kufurahia matunda ya kazi yake. Hapo ndipo mzaliwa wa Kibera, Mathare, Kangemi na Mukuru atashawishika kufanya bidii ya kujiondoa kwenye umaskini kwani atafahamu kuwa fanaka haiji tu kwa bahati na sibu ya sportpesa. Tutajua kuwa ukombozi wa tatu umefika wakati ambapo, itakuwa nadra sana kukutana na mtu maskini. Wakati ambapo makao yanayoitwa vitongoji duni hayatakuwepo tena na magereza kukosa wafungwa kwani uhalifu utakuwa umedidimia. Hayo yote ni ya baadaye lakini mwanzo ni kupambana na ukabila kwa udi na uvumba.

## Marejeleo


Mazrui, A. A. & Mazrui, A. M. (1989). *The power of Babel: Language and Governance in the African Experience.*University of Chicago Press.

Mulokozi, M. M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kisawhili*: OSW 105. Dar es salaam, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mutembei, A. (2012). *Karasi katika Fasihi*: *Nadharia Mpya ya Uhakiki wa Fasihi.* Dar es Salaam: TUKI.

Mushenyezi, A. (2003). *Twentieth Century Literary Theory*. Kampala: Makerere University Press.

Oxford Dictionary. (2018). Oxford University Press

Senkoro, F. V. M. K. (2011). *Fasihi: Mfululizo wa Lugha ya Fasihi*: Dar es Salaam: KAUTTU.

Walibora, K. (2014). *Nasikia Sauti ya Mama:* Sasa Sema Publications. Nairobi, Kenya.

Wamitila, K. W. (2000). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Msingi wa Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide Muwa Publishers.